# UVCCM yanogesha sherehe ya kuzaliwa Rais Samia

**Dodoma**
**NA FRED ALFRED**

KATIKA kusherekea siku ya kuzaliwa ya Rais Samia Suluhu Hassan, Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Dodoma wamempongeza Rais Samia kwa kuongeza serikali kwa amani, utulivu na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Akizungumza jana jijini hapa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Mussa Mwakitinya, alisema katika kutambua jitihada za Rais Samia, waliamua kuchangia damu katika kituo cha afya Makole na kugawa zawadi kwa wagonjwa ikiwemo sabuni za kuogea, biskuti na juisi.

"Tunampongeza Rais Samia kwa kuongeza mwaka, hatuna zawadi kubwa ya kumpa zaidi ya kumpongeza na kumuhakikishia vijana tutakuwa watu wema, tunafuata sheria za nchi, tutapinga rushwa, unyanyasaji wa kijinsia na matukio yote yasiyo na tija kwa jamii, tutaendelea kusismama na mama popote pale alipo, tunasema alipo mama na sisi vijana tupo.

Aliongeza kuwa: "Tunamshukuru Rais kwa kuendelea na hli miradi ya kimkakati kwani miradi hiyo ikikamilika itatoa fursa za ajira kwa Watanzania wengi zaidi ambao hawana ajira.

Alisema UVCCM inampongeza Rais Samia kwa kuimarisha mahusiano na mataifa mengine ambapo ameliheshimisha taifa.

"Mama aendelee kuchapa kazi vijana wako tuko pamoja na wewe, vijana tupo kamili kukutetea kwa lolote,"alisisitiza

Kwa upande wake, Katibu wa UVCCM Mkoa wa Dodoma, Ibrahim Kandumila, alisema lengo la kushiriki shughuli za kijamii katika siku ya kuzaliwa kwa Rais Samia ni kuendelea kuunga mkono jitihada zake katika kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo.

Alisema katika kumuunga mkono Rais Samia 0waliandaa keki mahususi, kuchangia damu, kuhamasisha uchanjaji na kutoa msaada wa mahitaji kwa baadhi ya wagonjwa waliolazwa katika Kituo cha Afya cha Makole.

"Lengo la kuja hapa ni kuunga mkono jitihada za mwenyekiti wetu wa chama ambaye pia ni Rais Samia, pia kutoa pole kwa wagonjwa ambao wamelazwa katika kituo hiki na kutoa damu kuokoa maisha ya watu ambao hupoteza maisha kwa ukosefu wa damu," alisema.

Naye, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Makole, Dk. Revocatus Baltazary, aliwashukuru vijana wa CCM kwa moyo wa kizalendo wa kuamua kwa hiyari yao kuchangia damu na kutoa hamasa kwa watu ambao hawaja chanja chanjo ya Uviko-19.

Alisema kiitaalamu tatizo la kukosa damu husababisha vifo vingi hususani kwa akina mama wajawazito ambao ndio wahitaji wakubwa wa damu.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kazi nzuri anayofanya, lakini pia na ninyi vijana kwa moyo mlioonyesha wa kuja kuchangia damu hakika mmefanya kitu kikubwa, pia msiache kuhamasisha jamii kujitolea damu ili tuendelee kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu,"alisema.

# Serikali yatoa madume ya ng'ombe borani kwa wafugaji

**Mkuranga**
**NA SCOLASTICA MSEWA**

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekabidhi madume matatu bora ya ng'ombe borani kwa vikundi vya wafugaji wa asili pamoja na majokofu 24 kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali wa mazao ya uvuvi kwa mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara, ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM (2020 – 2025) inayolenga kuwakwamua kiuchumi wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo mjini Mkuranga mkoani Pwani, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, alisema madume hayo ya ng`ombe yatakwenda kuboresha upatikanaji ng`ombe wa asili kwa wafugaji watakaoyatumia kupandikiza mbegu.

Kuhusu majokofu, Ulega alisema yatapunguza upotevu wa ubora wa mazao ya uvuvi hivyo kuongeza thamani, bei na kipato kwa wanawake wanaofanyabiashara ya mazao ya uvuvi.

Kwa upande wake, Mratibu wa miradi ya Pwani ya Bahari ya Hindi kwa miradi inayotekelezwa na WWF, Dk. Modesta Medadi, alisema wamekabidhi majokofu 24 kwa mgawanyo wa Wilaya ya Mkuranga majokofu 8, Kibiti majokofu 2 na injini ya boti ya uvuvi, Kilwa 5 na Mtwara Vijijini majokofu manne ikiwa ni mkakati wa kuwawezesha kina mama wajasiliamali wa bidhaa za uvuvi kuboresha kuongeza myororo wa thamani ya bidhaa za wajasiliamali.

Mkurugenzi wa Mbogo Ranchi Ubena Chalinze mkoani Pwani, Naweed Mulla, alisema ng'ombe hao bora wana thamani ya sh. milioni 15 wametoa kwa jamii hiyo ya wafugaji asili kuboresha ng'ombe wa asili.

"Ng'ombe hawa aina ya borani watakapozalishwa majike watakuwa bora kwenye uzalishaji wa mazao ya mifugo ikiwemo kiwango kikubwa cha maziwa, nyama, uhimulivu dhidi ya magonjwa na hali ya mazingira ya mikoa yetu," alisema.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Nassir Ally, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kusaidia na kuwaendeleza wafugaji na wajasiriamali wa bidhaa za uvuvi nchini.

UHURU UK5.



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akikabidhi madume bora ya ng'ombe aina ya Borani kutoka Mbogo Ranchi kwa vikundi vya wafugaji asili wa Wilaya ya Mkuranga ili kuzalisha ng'ombe chotara wenye ubora kwa wafugaji asili kupandisha majike yao ili waje kupata tija katika ufugaji wao. (Picha na Scolastica Msewa).

Scanned with CamScanner

historia kwa kuwa benki ya kwanza nchini kupata faida baada ya kodi ya Sh bilioni 210.

Taarifa ya matokeo ya mwaka mzima wa 2021 imesema faida kabla ya kodi ilikuwa Sh bilioni 420, ongezeko la asilimia 41 kwa mwaka kutoka Sh bilioni 301.

Akizungumzia mafanikio hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema anajivunia matokeo waliyoyapata kama timu na kuamini kuendelea kuwa na ukuaji endelevu wa biashara.

"Ukuaji mkubwa wa biwa kwa uwiano wa gharama na mapato hadi asilimia 47 kutoka asilimia 51 mwaka 2020, kiwango ambacho kipo ndani ya ukomo wa kibenki wa asilimia 55.

"Usimamizi makini wa mikopo na uhusiano mzuri na wateja uliboresha ubora wa jumla wa mali za benki na kufanya uwiano wa mikopo chechefu kupungua hadi asilimia 3.2 mwezi Desemba mwaka 2021, kiwango ambacho ni kidogo kulinganisha na takwa la kikanuni ya asilimia tano," taarifa ilibainisha.

Jumla ya mikopo iliyo-

uliifanya NMB kuwa benki ya kwanza kuwa na mfuko maalumu wa kuukopesha mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Mafanikio ya ukuaji wa NMB na mchango wake mkubwa kwenye uchumi wa Tanzania umeendelea kuifanya kinara wa ubora nchini kupitia tuzo mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Mwaka 2021, Benki ya NMB ilitunukiwa tuzo saba za kimataifa ikitangazwa kuwa Benki Bora na Salama Zaidi nchini Tanzania.

HABARI LEO UK 7.

# Serikali yatoa msimamo biashara ya punda

**Na Sifa Lubasi**

SERIKALI imesema haitatoa kibali cha biashara ya punda na mazao yake ikiwamo uchinjaji kwa wawekezaji kutoka China hadi wanyama hao watakapofikia idadi ya milioni 10.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mfugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga alitoa msimamo huo wakati wa mkutano wa tathmini baada ya serikali kusitisha uchinjaji wa punda katika kampuni za Huacheng International LTD ya Dodoma na Fang Hua Investment CO LTD ya Shinyanga.

Profesa Nonga alisema jike la punda linabeba mimba miezi 13 na likizaa linalea mtoto kwa miaka mitano na kwamba punda mmoja kwa miaka 10 anaweza akazaa mtoto mmoja au asizae kabisa.

Alisema wawekezaji wakati wanaanza kuchinja punda miaka ya 2016 hadi 2017 walikuwa wanachinja punda hao idadi yoyote pasipokuwa na ukomo.

"Walikuwa wanachinja idadi ya punda 400 kwa siku, idadi ya punda waliopo Tanzania hawazidi hata 700,000 kwa wakati ule na waliendelea kuchinja zaidi ya punda 400 kwa siku, ikafika wakati punda hao wakaisha," alisema Profesa Nonga.

Alisema Oktoba mwaka jana, aliyekuwa waziri wa wizara hiyo, Mashimba Ndaki alizuia uchinjaji wa punda nchini baada ya wawekezaji kukiuka masharti.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Dk Jonas Kizima, alisema yeye binafsi alishiriki katika utafiti kwa kushirikiana na taasisi tatu kikiwemo Chama cha Kutetea Haki za Mifugo Arusha (ASPA), kuangalia ni namna gani punda wanafugwa katika jamii.

"Tulibaini biashara ya uchinjaji punda imeshamiri, utafiti ulionesha asilimia 68 ya watu waliohojiwa katika wilaya za Iringa, Chemba, Monduli na Arusha walio wengi hawapendi uchinjaji wa punda," alisema.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2016 hadi 2019 baada ya kufanya tathimini walikuta punda waliochinjwa ni 88,312.

Mkurugenzi Mtendaji wa ASPA, Livingston Masija alisema wanataka punda waendelee kuwasaidia wananchi katika shughuli za kila siku kama kuchota maji, kubeba matofali, kuni na mazao kutoka shambani kupeleka nyumbani," alisema.

Scanned with CamScanner

# Madiwani walalamika kuitwa

Na Raymond Mihayo, Kahama

BARAZA la Madiwani wa Manispaa limelalamika vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi vya kuwaita madiwani mizigo kupitia mitandao ya kijamii.

"Sisi madiwani wa Manispaa husika tunaomba tuheshimiane, kwani tumekuwa tukikaa vikao na kupitisha maazimio mengi, kwa hiyo tunaomba tusidharauliane katika kazi tunazofanya kwa maslahi ya wananchi katika maeneo yetu."

Hiyo ni kauli ya Diwani wa Majengo, Bernard Mahongo katika kikao cha Baraza kilichokaa juzi kupitisha mapendekezo ya bajeti ya Manispaa kwa mwaka 2022/23.

Mahongo alisema wamekuwa wakikaa na makabrasha zaidi ya wiki, wakiyapitia na kurekebisha panahitajika na kuongeza kuwa maendeleo ya Kahama hayafanywi na mtu mmoja ambaye ni Mkurugenzi wa Manispaa.

Alisema wamechoka kuitwa mizigo na kutukanwa kwenye mitandao inayojiita Kahama Political, kwani katika wilaya hii madiwani wamefanya mengi ya maendeleo, na yenye manufaa kwa wananchi.

Hata hivyo, Mahongo alisema hapana budi kuheshimiana na pale Mkurugenzi anaposifiwa kwa kufanya maendeleo, aseme si peke yake, bali nyuma yake kuna madiwani ambao wamefanya kazi kubwa.

Diwani wa Kahama Mjini, Hamidu Kapama alisema katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka huu, nguvu kubwa

* RAIA MWEMA UKB *

# Wafugaji walioingiza mifugo waonywa

Na Kija Elias, Mwanga

SERIKALI wilayani hapa, imewataka wafugaji walioingiza mifugo yao kutafuta malisho bila utaratibu, waondoke haraka.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya, Abdallah Mwaipaya, kwenye kikao maalumu cha Baraza la Madiwani kilichopokea, kujadili na kupitisha bajeti ya halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mwaipaya alisema kuna makundi makubwa ya ng'ombe ndani ya wilaya hiyo yakitafuta malisho, jambo ambalo limesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

"Wilaya ya Mwanga tumelemewa na mifugo kwa sasa, hatuna tena maeneo ya kukusanya mifugo inayokuja kutoka maeneo jirani kwa lengo la kutafuta malisho.

"Nimemwagiza ofisa tarafa na ofisa mifugo wa wilaya kuwaandikia barua ya kuwaeleza wenyeviti wa vijiji na kata, kusitisha utoaji vibali vya kuruhusu kuingiza mifugo ndani ya wilaya hii kwa sasa," alisema Mwaipaya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Mwajuma Nasombe, alisema kwa miezi michache iliyopita, wilaya ya Mwanga ilipata mvua za vuli na hivyo kusababisha nyasi kuota na hivyo kuwa kimbilio la wafugaji kuleta mifugo yao ndani ya wilayani.

"Kutokana na mvua chache za vuli zilizoonesha hivi karibuni katika wilaya yetu, nyasi nyingi zimeota takribani maeneo yote ya Mwanga, jambo lililofanya wafugaji kuleta mifugo yao bila utaratibu hususani katika kata za Jipendea, Mgagao na Kalambandea na kusababisha makundi makubwa ya mifugo," alisema Nasombe.

Alisema mifugo hiyo walibaini imekuwa ikitoka Arusha, Monduli na Simanjiro ambapo Januari 25 mwaka huu takribani ng'ombe zaidi ya 50,000 ziliingizwa katika wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa Nasombe mifugo ambayo imekuwa ikiripotiwa kufa ndani ya wilaya hiyo si ya wilaya ya Mwanga, ni ng'ombe waliosafirishwa umbali mrefu bila kupata malisho ya kutosha, wamekuwa wakifa, ambapo kwa siku ng'ombe 20 hadi 30 zinakufa kutokana na kutembea umbali mrefu bila malisho.

Kaimu Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Wilaya ya Mwanga, Email Mkemwa, alisema kutokana na maeneo mengi kuathiriwa na ukame, wafugaji wamekuwa wakilazimika kuleta mifugo yao katika wilaya ya Mwanga kutokana na kuwepo nyasi nyingi.

Mkwema alisema kuwapo makundi makubwa ya ng'ombe, kuna hatari kubwa ya kutokea milipuko ya magonjwa ya mifugo katika wilaya hiyo.



# Wachimbaji 250 wakimbilia CCM

Na Dotto Mwaibale, Singida

WAFANYAKAZI zaidi ya 250 wa mgodi wa Mpipiti katika kata ya Mudida wilayani hapa akiwamo aliyekuwa mgombea udiwani wilayani Maswa, Simiyu, Adolf Saida (Chadema) wamejiunga na CCM.

Akizungumza baada ya kupokewa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Singida, William Nyalandu aliyekuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya CCM yaliyoandaliwa na Umoja wa Vijana (UVCCM), Saida alisema wameamua kujiunga na chama hicho, baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mmoja wa wakurugenzi wa mgodi huo, Mussa Maduhu alisema changamoto kubwa waliyonayo ni kujengewa daraja, kukatika umeme unaokwamisha utoaji maji mengi maduarani na gharama kubwa ya kupeleka miti ya kufungia maduara kwa usalama wa kazi.

Alisema mgodi huo unakadiriwa kuwa wa pili kwa uzalishaji kimkoa, b
mgodi wa Sekenke wilayani Irar

"Tumekuwa na changamoto n
lakini utatuzi umekuwa ukichu
muda mrefu kwa ahadi nyingi
za baadhi ya viongozi waliofika
mgodini kujua changamoto ze
alisema Maduhu.

Aidha, alishukuru wachimb
kwa kufanya kazi kwa bidii ka
mazingira ya amani na utuliv
hali hiyo ndiyo imekuwa ikic
kupata madini mengi, na kui
Serikali mapato na wao kuin
kiuchumi.

Akizungumza katika maad
hayo, Nyalandu aliwaomba
utakapowadia muda wa uch
viongozi mapema mwezi uj
wenye weledi ili kumsaidia
Rais Samia.

Nyalandu aliwataka wan
kuimarisha chama kwa ku
na kulipa ada upitia mfum
kielektroniki na kuhimiza

Scanned with CamScanner